East African Journal of Swahili Studies, Volume 7, Issue 1, 2024
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1912




East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 7, Issue 1, 2024
Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Chanzo cha Makosa ya Kiisimu Miongoni mwa Wanafunzi Wanaozungumza Lahaja ya Kigichugu Wanapojifunza Kiswahili Kama Lugha ya Pili

*Nancy Wanja Njagi[1*] na Dkt. David Kihara, PhD[1]*

[1] Chuo Kikuu cha Kenyatta, S. L. P. 43844-00100, Nairobi, Kenya.
[*] ORCID ID: https://orcid.org/0009-0003-4030-0841; Barua pepe ya mawasiliano: nancywanja127@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1912**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*07 Mei 2024*

**Istilahi Muhimu**:

*Sintaksia Finyizi, Tafsiri Sisisi, Ujumlishaji Mno, Kishamirishi, Kibainishi, Kipatanishi.*

**IKISIRI**

Kiswahili kimekuwa muhimu sana hata kabla ya ujio wa wakoloni nchini Kenya hasa katika kuendeleza mawasiliano. Kabla ya wakoloni, Kiswahili kilitumika katika maeneo ya Pwani kuendeleza mawasiliano ya kibiashara miongoni mwa wakaazi wa Pwani na Waarabu. Biashara ilipoendelea kunoga na watu kutoka maeneo ya bara kuanza kushiriki katika biashara ya pale pwani, Kiswahili kilienea na matumizi yake yakapanuka. Licha ya kupanuka kimatumizi Kiswahili kimekubwa na changamoto nyingi, mojawapo ikiwa ni kuwepo kwa makosa ya kiisimu hasa kwa wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Hivyo basi utafiti huu ulikusudia kubaini chanzo cha makosa ya kiisimu miongoni mwa wanafunzi hasa wanaozungumza lahaja ya Kigichugu wanapojifunza kiswahili kama lugha ya pili. Uchunguzi huu uliendelezwa nyanjani na maktabani.Nyanjani ulitekelezwa katika shule za sekondari za kutwa katika kaunti ndogo ya Gichugu zilizoteuliwa kwa kutumia mbinu ya sampuli kimaksudi. Wanafunzi walioshiriki katika shule hizi walichaguliwa kwa kutumia mbinu ya usampulishaji wa kinasibu pale ambapo walipatiwa nambari kinasibu na waliopata nambari moja hadi sita kuteuliwa. Data ya utafiti huu ilikusanywa kwa kutumia hojaji, na masimulizi na kuwasilishwa kupitia majedwali na maelezo. Matokeo ya utafiti huu yalidhihirisha kuwa wengi wa wanafunzi katika shule za upili za kutwa katika eneo la Gichugu hujifunza Kigichugu kama lugha yao ya kwanza. Isitoshe, wengi huanza kutumia Kiswahili wanapojiunga na shule. Isitoshe, utafiti huu ulidhihirisha makosa mengi ya kiisimu (yaliyovunja kanuni za nadharia ya Sintaksia Finyizi) yaliyotokana na lahaja ya Kigichugu. Vyanzo vya makosa haya ambavyo vinaegemea kwa kiasi kikubwa kwa L1 ni : uhamishaji wa mifumo ya kiisimu, tafsiri sisisi, na ujumlishaji mno.

**APA CITATION**

Njagi, N. W. & Kihara, D. (2024). Chanzo cha Makosa ya Kiisimu Miongoni mwa Wanafunzi Wanaozungumza Lahaja ya Kigichugu Wanapojifunza Kiswahili Kama Lugha ya Pili. *East African Journal of Swahili Studies*, *7*(1), 212-223. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1912.

**CHICAGO CITATION**

Njagi, Nancy Wanja and David Kihara. 2024. "Chanzo cha Makosa ya Kiisimu Miongoni mwa Wanafunzi Wanaozungumza Lahaja ya Kigichugu Wanapojifunza Kiswahili Kama Lugha ya Pili". *East African Journal of Swahili Studies* 7 (1), 212-223. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1912.

**HARVARD CITATION**

Njagi, N. W. & Kihara, D. (2024) "Chanzo cha Makosa ya Kiisimu Miongoni mwa Wanafunzi Wanaozungumza Lahaja ya Kigichugu Wanapojifunza Kiswahili Kama Lugha ya Pili", *East African Journal of Swahili Studies*, 7(1), pp. 212-223. doi: 10.37284/jammk.7.1.1912

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

**IEEE CITATION**

N. W. Njagi & D. Kihara "Chanzo cha Makosa ya Kiisimu Miongoni mwa Wanafunzi Wanaozungumza Lahaja ya Kigichugu Wanapojifunza Kiswahili Kama Lugha ya Pili", *EAJSS*, vol. 7, no. 1, pp. 212-223, May. 2024.

**MLA CITATION**

Njagi, Nancy Wanja & David Kihara. "Chanzo cha Makosa ya Kiisimu Miongoni mwa Wanafunzi Wanaozungumza Lahaja ya Kigichugu Wanapojifunza Kiswahili Kama Lugha ya Pili". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 7, no. 1, May. 2024, pp. 212-223, doi:10.37284/jammk.7.1.1912.

## UTANGULIZI

Kiswahili kimekuwa muhimu sana hata kabla ya ujio wa wakoloni nchini Kenya hasa katika kuendeleza mawasiliano. Kabla ya wakoloni, Kiswahili kilitumika katika maeneo ya Pwani kuendeleza mawasiliano ya kibiashara miongoni mwa wakaazi wa Pwani na Waarabu. Biashara ilipoendelea kunoga na watu kutoka maeneo ya bara kuanza kushiriki katika biashara ya pale pwani, Kiswahili kilienea na matumizi yake yakapanuka. Wakati wa ukoloni na hata baada ya Kenya kujipatia uhuru, Kiswahili kimeendelezwa na kupatiwa hadhi mbalimbali. Hadhi hizi ni kama vile; hapa Kenya, ni lugha rasmi na ya taifa (Mauti, 2022). Licha ya hilo, imevuka mipaka ya Kenya, ni ya Kimataifa na inatumika na takriban watu milioni 120 ulimwenguni, Njoka (2021). Lugha hii imepanuka sana nje ya mipaka ya Kenya, hivi kwamba ni lugha ambayo ilipendekezwa na wengi kuwa lugha ya umajumui wa kiafrika, (Mulokozi, 2018), pia kimehusishwa na maendeleo ya kiteknolojia mathalani kuwepo kwa Google Swahili na toleo la Microsoft Office la Kiswahili. Zaidi ya kuwa lugha ambayo inatumika sana nchini Kenya na ulimwenguni, lugha hii imepewa pia dhima ya kufundishwa na kutahiniwa.

Katika mtaala wa 8-4-4 uliopendekezwa na tume iliyoongozwa na Mackay (1981) somo la Kiswahili lilifanywa la lazima na la kutahiniwa katika shule za sekondari na msingi (Hwang, 2011). Dhima hii haijapuuzwa hata katika mtaala wa umilisi pale ambapo somo la Kiswahili ni la lazima na la kutahiniwa katika daraja ya chini na juu ya shule za upili na shule za msingi. Hata hivyo mtaala huu umejumuisha ufundishaji wa lugha za kiasili na matumizi ya lugha hizi kufundisha katika viwango vya chini vya elimu (PP1 na PP2). Katika viwango hivyo vingine; shule ya msingi na ya upili (daraja ya chini na juu) lugha za kiasili ni za uchaguzi lakini Kiswahili ni somo la lazima. Kwa kuzingatia haya, ni dhahiri kuwa Kiswahili kinatumika sana nchini Kenya na hata ulimwenguni, hivyo basi ni muhimu kuzungumza na kujifunza kutumia Kiswahili sanifu. Jambo hili lilitupa mchocheo wa kutafiti chanzo cha makosa ya kiisimu miongoni mwa wanafunzi hasa wanaozungumza lahaja ya Kigichugu wanapojifunza kiswahili kama lugha ya pili. Aidha, kumekuwa na tetesi kuhusu matokeo duni ya wanafunzi katika Kiswahili hasa katika mtihani wa shule za sekondari. Matokeo haya yasiyoridhisha ni sababu nyingine iliyotuchochea tuchunguze chanzo cha makosa haya ya kiisimu ambayo mwanafunzi hasa wanaozungumza lahaja ya Kigichugu hupata katika somo hili, na kuchangia matokeo duni.

## MBINU ZA UTAFITI

Ili kupata data ya utafiti huu tulitekeleza utafiti maktabani na pia nyanjani. Utafiti wa maktabani ulihusisha usomaji wa makala ya mtandaoni, vitabu, na majarida kuhusu ujifunzaji lugha na nadharia ya Sintaksia Finyizi iliyoongoza utafiti huu. Utafiti wa nyanjani ulifanywa katika shule za sekondari za kutwa katika tarafa ya Gichugu, kaunti ya Kirinyaga. Eneo hili lina kata tano ambazo ni Kabare, Ngariama, Njukiini, Karumandi, na Baragwi na shule ziliteuliwa kutoka maeneo haya kwa sababu ndiko kuna wazungumzaji asilia wa Kigichugu. Isitoshe wanafunzi wengi wa shule za kutwa wamezaliwa na kulelewa katika eneo hili ikilinganishwa na wale wa shule za bweni. Katika uchaguzi wa shule za kutwa za kufanyia utafiti, tulitumia mbinu ya sampuli kimaksudi pale ambapo tuliteua shule mbili za kutwa katika kila kata tukizingatia utendaji wao katika mtihani wa KCSE wa Kiswahili. Tulichagua shule ya kwanza na ya mwisho katika kata hizo.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

East African Journal of Swahili Studies, Volume 7, Issue 1, 2024
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1912

**Jedwali 1: Utendaji wa wanafunzi katika mtihani wa KCSE**

| Eneo | Shule | Wasi-Chana | Wa-Vula-Na | Wanafunzi Wote | Alama za Wastani (2022) | Alama za Wastani (2021) | Alama za Wastani (2020) | Nambari |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Baragwi | Rwambiti | 43 | 55 | 98 | 5.735 | 5.171 | 3.568 | 1 |
| Baragwi | Kiamwathi | 41 | 73 | 114 | 5.434 | 4.495 | 5.140 | 2 |
| Njukiini | Gacatha | 49 | 59 | 108 | 4.935 | 3.759 | 4.459 | 3 |
| Karumandi | Kavote | 47 | 62 | 109 | 4.789 | 5.626 | 5.720 | 4 |
| Njukiini | Kianyambo | 19 | 27 | 46 | 4.740 | 3.166 | 4.050 | 5 |
| Njukiini | Gaciongo | 14 | 8 | 22 | 4.429 | 3.227 | 2.733 | 6 |
| Kabare | St.Louis Nyagithuci | 10 | 20 | 30 | 4.267 | 3.615 | 2.882 | 7 |
| Kabare | OLCS Rukenya | 71 | 90 | 161 | 4.244 | 3.259 | 4.078 | 8 |
| Karumandi | Mucagara | 44 | 37 | 81 | 3.988 | 3.069 | 3.944 | 9 |
| Njukiini | Kiaumbui | 19 | 17 | 36 | 3.890 | 3.050 | 4.500 | 10 |
| Kabare | Kianguenyi | 8 | 16 | 24 | 3.833 | 4.000 | 2.826 | 11 |
| Ngariama | Ngariama | 14 | 36 | 50 | 3.833 | 4.424 | 3.193 | 11 |
| Kabare | Gatugura | 20 | 35 | 55 | 3.800 | 3.097 | 3.350 | 13 |
| Baragwi | Kiandai | 13 | 20 | 33 | 3.788 | 3.765 | 4.813 | 14 |
| Njukiini | Karucho | 40 | 43 | 83 | 3.747 | 3.819 | 3.621 | 15 |
| Kabare | Ngungu | 21 | 19 | 40 | 3.700 | 3.138 | 3.946 | 16 |
| Kabare | Kimunye | 11 | 23 | 34 | 3.677 | 3.359 | 4.720 | 17 |
| Njukiini | Kanjuu | 13 | 17 | 30 | 3.310 | 3.266 | 3.080 | 18 |
| Ngariama | Githure | 5 | 17 | 22 | 3.272 | 2.686 | 2.761 | 19 |
| Ngariama | Mwanianjau | 7 | 10 | 17 | 3.138 | 2.737 | 2.688 | 20 |
| Baragwi | St.Mary Magdalene Githage | 10 | 19 | 29 | 2.517 | 2.481 | 3.200 | 21 |

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

East African Journal of Swahili Studies, Volume 7, Issue 1, 2024
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1912

Hivyo basi tulifanya utafiti katika shule zifuatazo:

**Jedwali 2: Shule za kwanza na za mwisho katika kila eneo**

| | Shule | Alama ya wastani |
|---|---|---|
| Baragwi | Shule ya Upili ya Kutwa ya Rwambiti | 5.735 |
| | Shule ya Upili ya Kutwa ya St.Mary Magdalene Githage | 2.517 |
| Njukiini | Shule ya Upili ya Kutwa ya Gacatha | 4.935 |
| | Shule ya Upili ya Kutwa ya Kanjuu | 3.31 |
| Karumandi | Shule ya Upili ya Kutwa ya Kavote | 4.789 |
| | Shule ya Upili ya Kutwa ya Mucagara | 3.988 |
| Kabare | Shule ya Upili ya Kutwa ya St.Louis Nyagithuci | 4.267 |
| | Shule ya Upili ya Kutwa ya Kimunye | 3.677 |
| Ngariama | Shule ya Upili ya Kutwa ya Ngariama | 3.833 |
| | Shule ya Upili ya Kutwa ya Mwanianjau | 3.138 |

Katika uteuzi wa wanafunzi tulichagua wanafunzi wanaozungumza Kigichugu kama lugha ya kwanza. Licha ya hilo tulichagua wanafunzi katika kidato cha tatu na cha kwanza kwa sababu umilisi wa wanafunzi wa kutumia lugha katika kidato cha kwanza haujakomaa ilhali wanafunzi katika kidato cha tatu wana ukomavu wa kutumia lugha. Tuliteua sampuli ya wanafunzi sita katika kila shule , hivyo basi kwa jumla tulikuwa na sampuli ya wanafunzi sitini. Katika uteuzi wa wanafunzi tulitumia usampulishaji wa kinasibu pale ambapo tulipatia wanafunzi nambari kinasibu na kuteua waliopata nambari moja hadi sita. Katika uchunguzi huu mbinu ya hojaji iliyokuwa na maswali ya sarufi na matumizi ya lugha ilitumiwa miongoni mwa wanafunzi. Fauka ya hilo, walipewa insha ambazo zilisahihishwa kwa makini ili kujaribu kupata makosa ya kisintaksia wanayofanya na kuyaainisha kwa makundi kulingana na aina za makosa yale na kisha kuyatumia kuchunguza chanzo chake.

## MATOKEO NA MAJADILIANO YA MATOKEO

### Demografia ya Watafitiwa

Katika sehemu hii tutaweka wazi sifa za kibinafsi za walioshiriki katika utafiti huu. Sifa hizi ni kama vile: lugha yao ya kwanza, wakati walianza kutumia Kiswahili, na lugha zingine ambazo wanafahamu isipokuwa Kigichugu.


### Lugha ya Kwanza

Hojaji sitini zilisambazwa katika shule kumi za upili za kutwa katika eneo bunge la Gichugu. Wanafunzi wote sitini walioshiriki, walikiri kuwa lugha yao ya kwanza ilikuwa Kigichugu; asilimia mia moja (100 %).

### Matumizi ya Kiswahili

Wakati wanafunzi waliofanyiwa utafiti walianza kutumia Kiswahili umebainishwa katika *mdwara 1*

**Mdwara 1: Wakati wanafunzi walianza kutumia Kiswahili**




 | This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.


Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1912

Utafiti huu ulibaini kuwa idadi kubwa ya wanafunzi 41(68%) walianza kutumia Kiswahili walipojiunga na shule. Hata hivyo, utafiti huu uligundua kuwa (mchoro 1) wanafunzi 19(32%) ya wanafunzi Wagichugu waliofanyiwa utafiti walianza kutumia Kiswahili kabla ya kujiunga na shule.

**Lugha Wanazojua**

Isipokuwa Kigichugu, lugha zingine ambazo watafitiwa walisema wanajua zimebainishwa katika *Grafu 2*.

**Grafu 2: Lugha wanazojua**




Isipokuwa Kigichugu wanafunzi wote sitini walisema wanajua Kiswahili na Kiingereza. Zaidi ya lugha hizi, mwanafunzi mmoja alisema anakijua Kiluhya (1), wanne Kiembu (4), wawili Kindia (2), wanne Kimeru (4), mmoja Kimwea (1), wawili Kikamba (2), na mmoja Kigiriama (1).

**Misingi ya Nadharia**

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ambayo inaweza kueleza ujuzi wa kisarufi ili kuweka wazi makosa ya kisarufi ambayo yanafanywa na wanafunzi Wakigichugu wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili na kubainisha chanzo cha makosa haya. Mtazamo huu ni Sintaksia Finyizi, uliyoasisiwa na Noam Chomsky mnamo miaka ya tisini (1995) kama marekebisho ya nadharia ya Utawala na ufungami. Noam Chomsky, alibomoa vijinadharia sita vya awali na akavitumia kama kanuni za sintaksia zinazotawala uhusiano wa kategoria za maneno, dhima ya sentensi na muundo wake. Ukiukaji wa kanuni hizi , hupelekea kuwepo kwa makosa ya kisarufi. Kanuni hizi ni kama vile kanuni leksia , utegemezi muundo, sheria ya uarifu, kanuni ya ufungami na kanuni ya ufasiri kamili .

**Makosa ya Kiisimu**

Ukiukaji wa kanuni za nadharia ya Sintaksia Finyizi hupelekea kuwepo kwa makosa ya kiisimu hasa ya kisintaksia (Chomsky, 2014). Kanuni hizi hutawala uhusiano wa kategoria za maneno, dhima ya sentensi na muundo wake. Kwa hivyo, ili kuweza kubaini makosa ya kiisimu yanayofanywa na wanafunzi Wagichugu, tutaanza kwa kufafanua muundo wa sentensi ya Kiswahili kulingana na nadharia ya Sintaksia Finyizi.

Uundajii wa sentensi ya Kiswahili unategemea kategoria za maneno, miundo ya virai na majukumu ya kisintaksia. Kulingana na nadharia ya Sintaksia Finyizi kuna kategoria nane za maneno ambazo ni: nomino, kielezi, kivumishi, kibainishi, kishamirishi, kitenzi, kipatanishi, na kihusishi, (Mwihaki, 2007). Kategoria za maneno na makosa yanayohusiana na kategoria hizi za maneno yalibainishwa kama ifuatavyo:

**Makosa ya Kategoria za Maneno**

***Nomino***

Nomino ni neno linalotaja mahali, kitu, tukio, tabia, mtu, au hali yeyote ya kitu. Kwa mujibu wa nadharia ya Sintaksia finyizi, hii ndiyo kategoria

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1912

ya kimsingi , na huwezi kutunga sentensi yoyote bila kuitumia, aidha ikiwa huru au imepatanishwa katika muundo (Chomsky, 1995). Mathalani; mkulima analima shambani ( nomino ni mkulima na ni kategoria huru ) ilhali katika sentensi hii, 'analima shambani', mofimu (a) ni kiima kinachopatanishwa katika muundo. Kategoria za nomino huainishwa kwa kuzingatia ngeli ambazo zimeainshwa kwa kutumia vigezo viwili; kigezo cha kisintaksia na cha kimofolojia. Kigezo cha kimofolojia huhusisha uainishaji wa nomino kwa kutumia mianzo ya nomino husika katika umoja na wingi

Mfano; Ngeli ya M **-** WA: **M**toto anacheka.

**Wa**toto wanacheka.

Uainishaji wa ngeli kisintaksia, huongozwa na kanuni ya ufungami, pale ambapo nomino huainishwa kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi, kwa mfano;

Ngeli ya A-WA: Mtoto **a**nacheka.

Watoto **wa**nacheka.

Katika utafiti huu hatutaangazia vigezo vyote viwili, tulijikita katika kigezo cha sintaksia. Uainishaji wa ngeli kwa mujibu wa kigezo hiki umewekwa wazi katika *Jedwali 3* na unaonyesha kuwa maneno yaliyo katika tungo hufungamanishwa ili kuleta upatanisho wa kisarufi.

**Jedwali 3: Ngeli za nomino za Kiswahili**

| | Ngeli | Vipatanishi | Mifano katika tungo | |
|---|---|---|---|---|
| | | | **Umoja** | **Wingi** |
| 1. | A – WA | a , wa | Mwalimu anacheka. | Walimu wanacheka. |
| 2. | U – I | U ,i | Mti umeanguka. | Miti imeanguka. |
| 3. | LI –YA | Li , ya | Gari limeuzwa. | Magari yameuzwa. |
| 4. | KI –VI | Ki, vi | Kiti kimevunjika. | Viti vimevunjika. |
| 5. | U – ZI | U , zi | Ukuta umebomolewa. | Kuta zimebomolewa. |
| 6. | YA | Ya , ya | Marashi yananukia. | Marashi yananukia. |
| 7. | U | U ,u | Uji umemwagika. | Uji umemwagika. |
| 8 | I | i, i | Chumvi ilimwagika | Chumvi ilimwagika. |
| 9. | I –ZI | I, zi | Nguo imefuliwa | Nguo zimefuliwa. |
| 10 | U – YA | U, ya | Ugonjwa ulidhibitiwa | Magonjwa yalidhibitiwa. |
| 11 | Ku | Ku ,ku | Kucheka kwake kunaudhi | Kucheka kwao kunaudhi |
| 12 | PA | Pa | Pahali hapa panavutia. | Pahali hapa panavutia. |
| | KU | Ku | Mahali huku kunavutia. | Mahali huku kunavutia. |
| | MU | Mu | Mahali humu mnavutia. | Mahali humu mnavutia. |

Makosa ya Wanafunzi Wagichugu ya Upatanisho wa Kisarufi (Ngeli za Nomino za Kiswahili)

- Ng'ombe yetu **i**natoa maziwa.
- Chumvi **i**lizingirua na nzi.
- Mahospitali **ya**lifurika.
- Kipepeo **ki**meruka.
- Nzi **i**likufa.
- Maji **i**nayotiririka.
- Mashule **ya**lifungwa.
- Makanisa **ya**lifungwa.
- Samaki **i**livuliwa.
- Kipepeo **wa**meruka.
- Nzi **iko** ndani ya choo.
- Samaki **i**meliwa.

Makosa yaWanafunzi Wagichugu katika Matumizi ya Nomino

- Kufungwa kwa **mashule**.
- **Mahospitali** yalifurika.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1912

- Wauguzi wengi kupata **mda** mgumu.
- **Migogo** ya ndani kwa ndani.
- Ukosefu wa **adhira.**
- Kupunguzwa kwa wanaoudhuria **sheree.**
- **Nafazi** za kazi kukosa
- Uongezekaji wa vifo.
- Kufungwa kwa **mashule.**
- Kufungwa kwa **makanisa.**
- Vijana walijiingiza katika unyuaji wa madawa ya kulevya.
- **Uingiliano wa watu** kulisababisha kufungwa kwa kanisa.
- **Walioadhilika** na ugonjwa huo.
- **Utumiaji wa** dawa za kulevya.
- Mwalimu amekaa mbele ya **jukua**.
- Nilifika kabla ya **wazili** wa masomo.
- Mwaka wa elfu **bili** kumi na tisa.
- Kazeti.

***Kitenzi***

Kategoria hii huhusisha maneno yanayoashiria kitendo na huwa na uhusiano na kielezi, nomino au kihusishi. Vitenzi vimegawanywa katika vikundi viwili; viarifu kama vile, lima, cheka na kopula kama vile, yu, kuwa, na ni (Radford, 1997). Viarifu hujisimamia kimaana na hufungama na vipatanishi ili kuarifu kinachofanywa au kufanyiwa nomino. Kopula nacho, ni kitenzi ambacho kinatumika kushirikisha kiima na kiarifu. Shina la kitenzi hufungamana na vipatanishi ili kutoa fasiri kamili katika tungo. Muungano huu huongozwa na sheria ya ufungami. Kanuni ya ufasiri kamili pia hutawala mahusiano haya, ya kitenzi na kipatanishi kwa sababu kila kipatanishi kinasheheni maana mahususi ambayo ni muhimu kwa kitenzi hicho.

Makosa katika Matumizi yaVitenzi ya Wanafunzi Wagichugu

- Juma **alimula** ng'ombe jana.
- **Nilimtega** samaki mkubwa.
- Chumvi nyingi **humwadhibu** mtu.
- Jitu **lilinitokelea** jana usiku.
- Mama **alistuliwa** na jitu jana jioni.
- Familia mingi ziliangamia kwa **kugaramia** wagonjwa.
- Watu **hawakuitikizwa** kutoka mijini.
- Wanafunzi nao **walikoma** kwa masomo yao.
- Ndoa kusabaratika.
- **Nilididimia** katika masomo**.**
- Jitu **lilitongezea** katika msitu wa Sagamoyo.
- Kupunguzwa kwa **wanaoudhuria** sheree.
- Biashara nchini Kenya **zilisimamishwa.**
- Talanta zao **Walitoesha** kazi.
- Kuku ilianza **kusikia** maumivu.
- **Aligonga** kengele.
- Fisi **aligongwa** na nyuki.
- Fisi na sungura walianza **kuongelelea** vile bibi zao **huwatuma** wakasirike.
- Sungura alimwambia fisi **watandike** bibi zao.
- Fisi **alimtandika** bibi yake na kiboko.

***Kipatanishi***

Kipatanishi ni kiambishi kinachofungama na shina la kitenzi kuwakilisha vijenzi vya kisarufi; hali, yambwa, njeo, ngeli ya kiima na nafsi

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1912

(Radford, 1997). Hivyo basi tuna vipera vitano vya vipatanishi.

**Jedwali 4: Vipatanishi**

| Aina | Mifano |
|---|---|
| Kipatanishi njeo | Ataenda sokoni. |
| Kipatanishi nafsi | Nimefika. |
| Kipatanishi ngeli | Vimevunjika. |
| Kipatanishi kauli | Limiwa. |
| Kitenzi kisaidizi | Alikuwa amepika. |

Kategoroia hii ni muhimu sana katika sintaksia na huongozwa na kanuni ya ufasiri kamili pamoja na ya ufungami.

Makosa ya Wanafunzi Wagichugu ya Vipatanishi

- Ng'ombe yetu **i**natoa maziwa.
- Nzi **i**likufa.
- Mashule **ya**lifungwa.
- Makanisa **ya**lifungwa.
- Samaki **i**livuliwa.
- Kipepeo **wa**meruka.
- Samaki **ha**kitoka majini hufa.
- **Na**likuwa na watoto sita.

***Vivumishi***

Haya ni maneno yanayotoa taarifa zaidi kuhusu nomino, mathalani kuhusu tabia ya nomino. Hivyo basi nomino huwa na ukuruba wa kisintaksia na vivumishi. Vivumishi aghalabu huchukua viambishi awali vya ngeli. Kuna kategoria tatu finyu za vivumishi ambazo ni; vivumishi vya umbo, tabia na sifa (Radford, 1997).

Makosa yaWanafunzi Wagichugu ya Vivumishi

- Binadamu alifaa kuzingatia kula chakula **kisafi.**
- Watu walifaa kuosha mikono kwa kutumia sabuni na maji **masafi.**
- Jitu huyu ni **mkubwa.**

***Vibainishi***

Kategoria hii huhusisha maneno yanayoashiria sifa zinazohusiana na nomino lakini hazijafungamana na nomino hiyo (Karingi, 2012). Sifa hizi ni kama vile; kuashiria kitajwa, umilikishi, uwakilishaji (pronomino) na idadi. Vipera vya kategoria hii vimeorodheshwa katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali 5: Vibainishi**

| Kategoria finyu | Mfano katika sentensi |
|---|---|
| Kimilikishi | Kiatu chake kilipotea. |
| Kiratibishi | Mtoto wa kwanza alikuwa shupavu. |
| Pronomino | Mimi ni shupavu. |
| Kiashiria/ kionyeshi | Kitabu kile kimeraruka. |
| Kiidadishi | Vitabu vingi vilinunuliwa. |
| Kiswalishi | Gari lipi linauzwa ? |
| Kijumlishi | Chakula chochote kitaliwa |

Makosa ya Wanafunzi Wagichugu ya Vibainishi

- Nilikula chakula **kiangu.**
- Familia **mingi** ziliangamia.
- Kuishi kwa huzuni na hofu **kotekote** nchini.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1912

- Vitu zinginezo.
- Ng'ombe wetu hutoa maziwa **mingi** sana.
- Jitu **huyu** ni mkubwa.
- Niliona **venye** jitu liruka.
- Maduka mingi.
- Ugonjwa **huyu** uliangamiza watu wengi.
- Baada ya mwezi **moja**.
- Unasikiliza **vyenye** unaambiwa.
- Mama yake alimwita mara **mingi.**

***Vielezi***

Haya ni maneno yanayotoa ufafanuzi zaidi kuhusu vitenzi ,vielezi vingine na vivumishi. Maneno haya hujibu maswali, vipi?, lini?, na wapi? Kategoria finyu za vielezi ni kama vile; vielezi vya namna, kadiri, wakati, na mahali. Vielezi huwa na ukuruba wa kisintaksia na vitenzi na vivumishi. Isitoshe maneno haya hujaliza maana za vitenzi, nomino na vivumishi.

Makosa ya Wanafunzi Wagichugu ya Vielezi

- Alitembea **kamwe kamwe** hadi nyumbani.
- Wanafunzi wengi waliathirika **sana sana** wanafunzi wa darasa la nane.

***Vihusishi***

Ni maneno yanayoonyesha uhusiano uliopo kati ya vitenzi na vijenzi vingine kama vile nomino na vielezi katika sentensi. Vihusishi vimeanishwa katika kategoria mbili finyu; vihusishi sahili (katika, kwa, ya) na vihusishi elezi (mama alienda **sokoni**). Kisintaksia, vihusishi sahili aghalabu hutanguliwa na nomino, kivumishi au kibainishi na hufuatwa na nomino au kibainishi (kipronomino), kwa hivyo ni nadra katika muundo wa sentensi kuanza au kumalizia na kihusishi (Adjer, 2003).

Makosa ya Wanafunzi Wagichugu ya Vihusishi

- Turudi manyumbani.
- Wanabiashara ilibidi waludi **mashambani.**
- Maafa ya watu **inchini.**
- Kuabudia manyumbani.
- Barabara za kutoka **mijini mikuu.**
- Walioajiriwa **madarasani.**
- Nzi wanaishi **kwenye** joto jingi.
- Kijana mtundu alimwaga chumvi **kwenye** sakafu.
- Nilifika nyumbani **mbele ya** ndugu yangu.
- Kukosa pesa **ya** matibabu.
- Nzi ameingia **kwa** chai.
- Manufaa **kwenye** mifugo.
- Karakana imejengwa **mkabala na** bwalo.
- Nzi ameruka **kwa** chakula.
- Watu walianza kufa **juu ya** njaa.

***Kishamirishi***

Kategoria hii hujumuisha maneno ambayo huungana na kishazi ili kukamilisha kishazi cha kwanza kwa kuonyesha uhusiano wa vishazi hivyo viwili. Vijopo vya vishamirishi ni; kishamirishi kirejeshi (amba -), kishamirishi unganifu ambavyo katika sarufi mapokeo viliainishwa kama viunganishi (na, ingawa, au, isitoshe, ama, ilhali, lakini) na pronomino husishi (kuwa, kwamba, ili, kuwa, muradi ) ambalo ni jopo la maneno yanayopanua wazo la kiima kwa kulihusisha na wazo la awali.

Makosa ya Wanafunzi Wagichugu ya Vishamirishi

- Korona ni ugonjwa hatari **ambayo** hudhuru afya ya binadamu.
- Ukosefu wa ajira **ambayo** ilisababisha watu kukosa pesa za kujikimu mahitaji yao.
- Ili aonekane **ama** anaweza chimba kisima.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1912

- Fisi alimtandika bibi yake **na** kiboko.
- Baba alikula ugali **na** nyama.
- Nilichapwa **na** kiboko.
- Nilifuta ubao **na** kifutio.
- Walibeba maembe **na** vikapu.
- Kusalimiana **na** mikono.
- Ali kadharika.

**Chanzo Cha Makosa**

Watafiwa wote katika utafiti huu walikiri kuwa lugha yao ya kwanza ni Kigichugu, hivyo basi walijifunza Kiswahili kama L2. Uchunguzi wa data katika utafiti huu umedhihirisha kuwa makosa ya kiisimu yaliyofanywa na wanafunzi wengi Wagichugu yalitokana na athari ya lugha ya kwanza. Lugha ya kwanza ya wanafunzi hawa iliathiri ujifunzaji wao wa Kiswahili , kiasi kuwa walihamisha dhana na mifumo ya kiisimu ya L1 hadi L2. Isitoshe walitafsiri maneno au kauli moja moja kutoka lugha ya kwanza na wengine wakajumlisha mno kanuni za lugha ya kwanza.

***Uhamishaji wa Mifumo ya Kiisimu***

Wanafunzi Wagichugu walihamisha moja kwa moja mifumo na dhana za kiisimu za lahaja ya Kigichugu kama vile ngeli, wingi wa maneno, vibainishi katika ngeli tofauti tofauti, udogo na ukubwa, suala lilopelekea kuwepo kwa makosa kama vile; ya ufungami.

**Jedwali 6: Uhamishaji wa Mifumo ya Kiisimu**

| Kosa | Tafsiri katika Kigichugu | Sahihi |
|---|---|---|
| *Ugonjwa huyu* uliangamiza watu wengi. | Mũrimũ *ũyu* nĩwaninire andũ aĩngĩ. | Ugonjwa *huu* uliangamiza watu wengi. |
| Kipepeo *ki*meruka. | kĩ βũrũtĩa ni*kĩr*arũgarũga. | Kipepeo *a*meruka. |
| *Ki*toto *k*ilianguka chini. (ukubwa) | Kĩana *Kĩ*raguire thi. | Toto *li*lianguka chini. |
| Samaki *i*livuliwa. | Θamaki *ĩ*rategirwe. | Samaki *a*livuliwa. |
| *Ka*paka *ka*lipotea jana (udogo). | *ka*ɲaũ *ka*lorire ĩgoro. | *Ki*paka *ki*lipotea jana. |
| *Makanisa ya*lifungwa. | *Ma*kanitha makĩβĩkwa. | *Kanisa zi*lifungwa. |
| *Mashule* nyingi zilifungwa. | *MaŠukuru* maingi makĩβĩkwa. | *Shule* nyingi zilifungwa. |

***Tafsiri***

Makosa mengine yalitokana na wanafunzi Wagichugu kutafsiri misamiati ya Kigichugu kiholeholela. Hili lilidhihirisha kuwa mwanafunzi aliwaza kwanza kwa lugha ya kwanza kisha akaanza kujaribu kuunda kauli za kiswahili lakini akajipata akifanya makosa ya kutumia msamiati usiofaa, nahau na hata muundo potofu wa sentensi.

**Jedwali 7: Tafsiri.**

| Kauli za wanafunzi | Kauli sahihi | Tafsiri katika Kigichugu |
|---|---|---|
| Umati wa watu *ulilolongana.* | Umati wa watu *uliandamana.* | Andũ aĩngĩ makĩroroŋgana. |
| Kufungia hewa. | *Kuzuia* hewa. | Ku β ĩ ŋg ĩ riria riera. |
| *huwatuma* wakasirike. | *Huwafanya* wakasirike. | *Matumaɤa* marakare. |
| Alimwambia fisi *watandike* bibi zao. | Alimwambia fisi *wachape* bibi zao. | Erire mbiti *matandike* atumia ao. |
| *Nilimtega* samaki mkubwa. | *Nilimvua* samaki mkubwa. | *Nindategirie* thamaki nene. |
| Alitembea *kamwe kamwe* hadi nyumbani kwa sungura. | Alitembea *moja kwa moja* hadi nyumbani kwa sungura. | Athire *rimwe rimwe* kinya muŠii kwa mbiti. |

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1912

### *Ujumlishaji Mno*

Ujumlishaji mno hujitokeza pale ambapo mwanafunzi anatumia kanuni za kisarufi za L1 kwa L2 bila kukusudia kwa kukosa kujua kanuni hizi zina mipaka (Norrish, 1983). Mathalani kuna vivumishi katika lahaja ya Kigichugu ambavyo huchukua viambishi vya ngeli lakini katika Kiswahili havichukui.

**Jedwali 8: . Ujumlishaji Mno**

| Kauli za wanafunzi | Tafsiri katika Kigichugu | Sentensi sahihi |
|---|---|---|
| Binadamu alifaa kula chakula *kisafi*. | Kitheru (ngeli ya KI –VI). | Binadamu alifaa kula chakula *safi*. |
| Alipaswa kutumia sabuni na maji *masafi*. | Abatie gutũmira mai *matherũ.* | Alipaswa kutumia sabuni na maji safi. |

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Utafiti huu ulidhamiria kubaini chanzo cha makosa ya kiisimu miongoni mwa wanafunzi hasa wanaozungumza lahaja ya Kigichugu wanapojifunza kiswahili kama lugha ya pili. Uchunguzi huu uliendelezwa nyanjani na maktabani.Nyanjani ulitekelezwa katika shule za sekondari za kutwa katika kaunti ndogo ya Gichugu zilizoteuliwa kwa kutumia mbinu ya sampuli kimaksudi. Wanafunzi walioshiriki katika shuke hizi walichaguliwa kwa kutumia mbinu ya usampulishaji wa kinasibu pale ambapo walipatiwa nambari kinasibu na waliopata nambari moja hadi sita kuteuliwa. Data ya utafiti huu ilikusanywa kwa kutumia insha, hojaji na masimulizi na kuwasilishwa kupitia majedwali na maelezo. Ilibainika kuwa japo, Kiswahili na lahaja ya Kigichugu (lahaja mojawapo ya lugha ya Kikuyu) zina mizizi sawa; ni za Kibantu, zinatofautiana katika baadhi ya vipengele vya kiisimu. Ubia huu wa vipengele vya kisarufi ndio uliosababisha baadhi ya makosa ya kiisimu ya wanafunzi wagichugu. Lugha hizi mbili hufanana katika baadhi ya vipengele vya kisarufi jambo lililofanya baadhi ya wanafunzi wakose kutambua tofauti finyu kati ya lugha hizi mbili.Vyanzo vingine vilivyopelekea kuwepo kwa makosa haya ya kiisimu miongoni mwa wanafunzi wagichugu ni; tafsiri sisisi na ujumlishaji mno.

Utafiti huu umeangazia chanzo cha makosa ya kiisimu hasa ya kisintaksia ya wanafunzi Wagichugu wanapojifunza Kiswahili kama L2. Matawi hayo megine ya kiisimu hayajaangaziwa, hivyo basi utafiti wa baadaye unaweza egemea katika matawi hayo mengine; fonolojia, mofolojia, semantiki, mathalani makosa ya kimofolojia ya wanafunzi Wagichugu.

## MAREJELEO


Adjer, D. (2003). *Core Syntax: A Minimalist Approach.* London: Oxford University Press. https://doi.org/10.1515/tlir.2003.014

Chomsky, N. (1995). Categories and transformations. *The minimalist program*, 219, 394.

Chomsky, N. (2014). *The minimalist program*. (20th Anniversary ed.). MIT press.

Hwang, K. D. (2011). Language Policy in Kenya With a Special Reference to Education. *Asian Journal of African Studies*, (30), 113-131.

Karingi, B. (2012). Ufunzaji na ujifunzaji wa vibainishi katika shule za upili Wilayani Kirinyaga. *Mtazamo wa sintaksia Finyizi, M.A Thesis,Chuo Kikuu cha Kenyatta*.

Mauti, G. M. (2022). Lugha Katika Katiba Ya Kenya: Ujitokezaji Wake Katika Utangazaji Wa Janga La Uviko-19 (*Doctoral dissertation, University of Nairobi*).

Mulokozi, M. M. (2018). Makala Elekezi: Kiswahili na Umajumui wa Kiafrika. *Mulika Journal*, 1(1).

Mwihaki, A. (2007). Minimalist Approach to Kiswahili Syntax. *Kiswahili a referred journal*, (70) 27.


This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1912

Njoka, A. (2021, Machi 17). *Uchambuzi: Kiswahili kinaweza kuwa Lingua Franka ya dunia*. https://www.mwananchi.co.tz/mw/kolamu/uchambuzi-kiswahili-kinaweza-kuwa-lingua-franka-ya-dunia-3010788.

Norrish, J. (1983). *Language Learners and their Errors.* London: Macmillan Press.

Radford, A. (1997). *Syntax: A Minimalist Introduction*.( 1st edition) Cambridge: Cambridge University Press.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.